5 **Kuratibu** (Coordinate) kwa ufanisi mipango mbalimbali inayotekelezwa na wadau ili kuwezesha kilimo biashara kwa vijana na wanawake





> “Kilimo ni Biashara

**scan kwa taarifa zaidi**

AJENDA 10/30
KILIMO NI BIASHARA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
**WIZARA YA KILIMO**

PROGRAMU YA
# JENGA KESHO ILIYOBORA
**(BUILDING A BETTER TOMORROW - BBT)**



bbt
Building a Better Tomorrow

## 1. UTANGULIZI

Programu ya Jenga Kesho iliyo Bora (Building a Better Tomorrow –BBT) ilizinduliwa tarehe 20 Machi, 2023 na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Uzinduzi huo ulifanyika katika shamba kubwa la pamoja (Block Farm) Chinangali, Dodoma. Programu ya BBT inalenga kuzalisha ajira zenye staha; Kuongeza uzalishaji na tija; Kuimarisha usalama wa chakula nchini; Kuongeza mchango wa sekta ya kilimo kwenye Pato la Taifa (GDP); na Kuimarisha hali ya Maisha ya jamii ya Watanzania kwa ujumla.

Utekelezaji wa programu hii unahusisha Serikali, Sekta Binafsi, na Washirika wa Maendeleo (DPs). Programu inalenga kufikia malengo yaliyobainishwa katika Sera, Mikakati na Mipango ya Kitaifa ikiwemo: Dira ya Taifa (TDV 2050); Sera ya Kilimo (2013); Mpango wa Kukuza Sekta ya Kilimo kwa 10% ifikapo 2030 (Ajenda 10/30); na Mpango Kabambe wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo (Tanzania Agriculture Master Plan 2050). Mipango na Mikakati hiyo inatambua nafasi ya sekta ya kilimo katika kutengeneza ajira kwa vijana na kuchangia katika Pato la Taifa.

Programu inalenga kutoa suluhisho katika changamoto mahususi zinazowakabili Vijana na Wanawake katika Sekta ya Kilimo nchini ambazo ni: Upatikanaji wa ardhi ya Kilimo; Upatikanaji wa mitaji; Upatikanaji wa teknolojia bora za kilimo; na Ufikiaji wa Masoko.




## 2. FURSA ZILIZOPO KUPITIA PROGRAMU YA BBT

Program inafadhiliwa na serikali na wabia wa maendeleo, hadi sasa Serikali kwa kushirikiana na AfDB, AGRA, IFAD na Benki ya Dunia imewezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya utekelezaji wa Programu katika maeneo yafuatayo:

**i.** Upatikanaji na uendelezwaji wa mashamba makubwa;

**ii.** Uongezaji thamani wa mazao ya kilimo

**iii.** Upatikanaji wa mikopo yenye riba nafuu kwa Vijana na Wanawake kuwekeza katika Kilimo;

**iv.** Uchimbaji wa Visima na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba makubwa na wakulima wadogo; na

**v.** Utoaji wa huduma za ugani (mafunzo na pembejeo za kilimo) kwa wakulima.



## 3. MALENGO YA KIMKAKATI YA KITAIFA YA UTEKELEZAJI WA BBT

i. Kutengeneza ajira kwa vijana na wanawake;

ii. Kuimarisha uzalishaji na tija kwenye kilimo;

iii. Kuinua hali ya kiuchumi na usalama wa chakula nchini

### Programu ya BBT itafikia malengo haya kupitia nguzo kuu 5 ambazo ni:

1. **Kuhamasisha** (Inspire) kwa kubadili mtazao kuhusu kilimo;
2. **Kuwajengea Uwezo** (Empower) vijana na wanawake kwa kuwapatia mafunzo ya kilimo Biashara kwa vitendo na matumizi ya teknolojia za kisasa katika kilimo;
3. **Kushirikisha** (Engage) vijana na wanawake katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo.
4. **Kuwezesha** (Enable) vijana na wanawake katika kilimo biashara, kwa kuboresha mazingira ya biashara pamoja na nyenzo muhimu za kilimo ikiwemo: kumiliki ardhi, kuwapatia mitaji, na kuwaunganisha na masoko; na